# Mwongozo wa mfukoni kuhusu kuzuia aina za kazi mbaya za watoto ndani ya migodi ya kuchimbia madini

## Kwao askari polisi jimboni Kivu ya Kusini

PACE

Partenariat Contre L'Exploitation Des Enfants

UKaid from the British people

# LENGO LA BUKU HILI LA MFUKONI

Buku hili linaelekeya vikosi vyote vya polisi ya Jamuhuri ya kidemokrasya ya Congo PNC wanao kabiliana na kupambana na Kazi za watoto ndani ya migodi ya madini, kwa upekekee askari polisi wa EPEPVS, wale wa PMH na polisi ya wilayani.

### *Buku hili lina jibu kwa upungufu mbili :*

- Kutambua na kuguswa ao kujibu kwa hali za kazi mbaya kwa watoto ndani ya migodi ya madini
- Kufahamu jukumu la kila mwigizaji anaekuwa ndani ya mpango wa kukinga haki za watoto

### Faida kubwa kwa moto

Kila kitendo wala hatua ya Polisi inapashwa kuweka kwa nafasi ya mbele **faida kuu ya mtoto**, ni kusema hivi, inabidi kuchukua kwa samani ili kujua hali gani, hitaji za pekee gani na msimamo wa mtoto.



# KUPINGANISHA AINA ZA KAZI MBAYA KWA WATOTO

### *Kwa nini kupiganisha kazi za watoto ?*

- Kwa ajili ya maisha na maendeleo ya mtoto
- Polisi inakuwa na jukumu la kukinga wanyonge
- Serkali ya RDC inapiganisha kazi kwa watoto na inalenga kuzikomesha
- Kutumika ndani ya migodi ya uchimbaji madini ni moja ya kazi za hatari kwa afya na ki akili kwa mtoto na inamzuwiya kwenda shuleni

### *Jukumu ya polisi ya taifa*

- Kuwatoa watoto ndani ya migodi ya uchimbaji madini wakiheshimu kwa makini haki za binadamu
- Kukinga haki za mtoto na kukamilisha faida yake kuu wakati wa kumuhudumia
- Kutia kwa nafasi ya mbele mazungumzo, uhimizaji na ushirika pamoja na wahusika wa ukingo wa mtoto

# KUTAMBUWA AINA ZA KAZI MBAYA KWA MTOTO

**_Mtoto ni nani ?_**

Kila yule ambaye hajafikia umri wa myaka 18 (kumi na nane) **ni mtoto**

**_Ni kazi gani ambazo zinakuwa mbaya zaidi kwa mtoto ndani ya migodi ya madini ?_**

- Kazi za kukazwa, utumwa
- Ukahaba wa watoto
- Kutumikisha watoto kwa kazi magendo wala za madawa za kulevya (bangi)
- Kazi za hatari kwa afya kama vile:
  - Kazi ndani ya shimu ya kuchimbia madini, chini ya udongo, chini ya maji, nafasi ambako kunafungwa
  - Kazi za kutumia mashini wala vifaa nzito tena vyenye hatari
  - Kazi kwa kutumia na bidhaa ya kemikali
- Kazi ambazo zinazuru maendeleo ya mtoto



# NI WAKATI GANI INABIDI KUJIBU IKIWA KUNAONEKANA KAZI HIZO MBAYA KWA WATOTO ?


Nafasi ya kuchimbia madini ni eneo ya hatari kwa kila mtoto anae patikana hapo. Mtoto anaetumika ndani ya migodi ya madini haiko muhusika wala mwenye makosa ila ni muhanga :

- Umaskini, kukosa fursa ao ukosefu ya kupata elimu
- Kosa ya mtu mzima kwa kazi ya kulazimishwa ukahaba, kazi za hatari ao aina nyingine mbaya zaidi ya ajira ya watoto

Polisi inapashwa kuweka kipaumbele makosa inayo kuwa na hatari kubwa kwa mtoto wala inayoweza kuleta madhara kwa maendeleo ya mtoto


Kisha kugundua kesi (kazi hiyo mbaya), polisi inapashwa kuwatosha watoto ndani ya migodi ya madini na kuwarudisha kwa usalama ndani ya jamaa zao wala kwenye vituo vya kijamii wakishirikiana na wahigizaji pia wanaokuwa na jukumu la watoto hao.

# KESI ZA KWELI ZINAZO HITAJI MAJIBU AO KUINGILIA KATI




***Kama mtoto analazimishwa kutumika, kufanya ukahaba, anatumikishwa kwa kazi haramu, akifanya kazi ya kuchosha wala inayo zuru maendeleo yake***

Hapo inakuwa kazi mbaya ya zaidi kwa watoto, ni kumaanisha kwamba inabidi kuingilia kati ao kutoa jibu haraka kwa ajili ya kumutoa mtoto huyo ndani ya hali hii, kumtolea msaada na kuanzisha uchunguzi ili wahusika wahazibiwe



***Utumiaji wa mercure wakati wa kusafisha dhahabu wala kuendesha kazi ndani ya shimu ya madini***

Hatari za ziada (kupita kiasi) kwa afya inahalalisha kuzingatia (kuchukua) kesi hiyi kama vile moja ya kazi mbaya kwa watoto



***Ikiwa kuna mtoto mchungaji ambae anaingia ndani ya eneo moja inayokuwa na mipaka, wala kama mtoto anauzisha bidhaa ndani ya eneo la uchimbaji madini***

Ingawa mtoto anaweza fanya kazi inayovumiliwa na myaka yake, anaweza anguka ndani ya shimu ya kuchimbia madini bila kujua. Inabidi kumuongoza inje ya eneo hilo la madini.

Kazi ya **uhimizaji, ya mazungumzo** na **ya ushirika** pamoja na wale wote wahusika ni ya muhimu kwa lengo la kubadilisha tabia mbaya

# NAMNA GANI KUMTOLEA MTOTO MSAADA KIKAMILIFU

## 1. Kutambua kesi na namna ya kujibu

- Kugundua kesi moja ya kazi mbaya kwa watoto kupitia hatuwa za **kuzuia** (doria, ziara ao mzunguuko)
- Polisi Kujibu wala kuingilia kesi hiyo bila vurugu ajili ya **kumuondoa mtoto ndani ya eneo la uchimbaji madini** na kumtia nafasi ya usalama
- Polisi kutoa **ripoti** kwa viongozi wake

## 2. Kupeleka kesi kwenye vituo husika

- Mtoto **anasikilizwa** na msaidizi kisheria kuhusu uchunguzi OPJ kwa kifupi, mtoto akiongozwa na msaidizi kijamii
- **Kumrejesha** na kumwongoza mtoto kufwatana na **haja zake maalum** (matibabu, kijamii na mengine)
- Ikiwezekana, **kuongeza** uchunguzi

## 3. Kufwatilia kesi pamoja na wengine waigizaji

- Kufwatilia mwenendo wa kesi pamoja na wengine waigizaji na kuendelea na kazi ya uhimizaji
- Kufwatilia kesi mbalimbali za makosa pamoja na mwendesha mashtaka pia pamoja na mahakama (tribinali) husika na mtoto

# NINI YA KUFANYA NA CHA KUEPUKA NA MTOTO

## Cha kufanya

- Kupokea mtoto, kujifahamisha na kueleza kazi na jukumu yako
- Kutumia mitindo nzuri ya maongezi na kusikiliza ili kuunda hali nzuri ya kutumainiana
- Kufanya iwezekanayo ili mbinu zako zikutane na haja kipekee za mtoto, myaka yake na hali yake

## Cha kuepuka

- Kumuweka mtoto kizuizini ao kumfunga
- Kutumia nguvu, unyanyasi ao vitisho
- Kukuwa na mawazo mabaya kuhusu hali ya mtoto na haja zake
- Tabia yoyote ambayo inazuru utu na akili ya mtoto



# HAKI NA MISINGI YA SHERIA

## Myaka kutokana na sheria (Sheria ya kazi, kipengele 6) :

- Kazi za watoto wa myaka chini ya 15 (kumi na tano) inakatazwa popote inchini DRC
- Myaka 15 mpaka 16, inabidi kuomba ruhusa kunako mahakama (tribinali) ya amani husika na mtoto
- Myaka 16 mpaka 18, kazi nyepesi peke yake na za kukinga afya yake ndizo anaweza endesha akiwa na ruhusa ya wazazi ao mlezi wake. Myaka kisheria ya kufanya mkataba ao makubaliano ya kazi ni 18.

## Aina aya kazi mbaya kwa watoto (sheria ya mwaka 2009 kuhusu ukingo wa mtoto, kipengele 53) :

- Kazi za kukazwa na hali yote ya utumwa
- Ukahaba
- Kutumikisha mtoto kwa kazi za kimagendo
- Kazi zote za kuzuru kwa afya, kwa ukoo, kwa usalama, kwa maendeleo, kwa heshima na tabiya ya mtoto

# HAKI NA MISINGI YA KISHERIA

## Mkosaji :

- Yoyote anaehuzuria kwa aina za kazi mbaya za watoto anaajibika kufungwa jelani kwa myaka 3 (tatu) na kulazimishwa malipo faini ya pesa elfu miya moja hadi elfu miya mbili (100 hadi 200 000) franga za Congo, art. 187)
- Kila anaehusika kujibu kwa swala hili akijizuiya kufanya kazi yake, analazimishwa kulipa faini ya pesa elfu miya moja hadi elfu miya mbili amsini (100 hadi 250 000) franga za Congo, art. 19

## Kazi za uchimbaji madini kiyolela (sheria ya madini, art. 299 bis) :

- Madini zinachimbwa ndani ya eneo ambapo panakuwa ukeukaji wa haki za watoto ni eneo isiyokubaliwa tena ya hatari
- Madini haziwezi kuchimbwa wala kuuzishwa. Kipengele 299 kinalazimisha Malipo ya faini ya pesa elfu kumi (10 000 USD) kwa siku kwa mchimbaji na mwenye kuuzisha analipa mara tatu thamani ya madini hiyo



# HAKI GANI ZA MTOTO INABIDI KUKINGA

- **Haki ya maisha, ya afya na ya maendeleo**
- **Haki ya uadilifu na ya usalama**
- **Haki ya maadibisho**
- **Haki ya sheria na kulipwa haki zao zilizo pokonywa**
- **Haki kwa kauli na kusikilizwa**
- **Haki ya kukingwa zhidi ya ubaguzi wowote**
- **Haki kwa usiri**

## Wanao husika na ukingo wa mtoto

### VITUO VYA MAWASILIANO VYA POLISI

**PMH:** 0972220664
**EPEPVS:** 0846870047

### MAHITAJI YA MATIBABU

**Fondation Panzi:** 0991688521
**Hôpital:** 0991141014

### MAHITAJI YA KIJAMII NA HUDUMA ZA KIUFUNDI

**Assistants sociaux:** 0997715007
**SAEMAPE:** 0819749502

### MAHITAJI ZA SHERIA

**Tribunal pour enfants:** 0993123531
**Parquet:** 0997044049

### KUREJESHWA NA UTETEZI

**World Vision:** 0991405860
**OBC Tupendane:** 0991793896
**RECOPE:** 0991009556
**Groupe de Travail:** 0994541218



## ANDIKO

“Uchapishaji huu umefadhiliwa na UK Aid, mpango wa maendeleo wa serkali Waingereza. Hata hivyo, maoni iliyotolewa ni ya waigizaji na haimaanishe kikamilifu siasa ki rasmi ya serkali ya Waingereza”.

**Mwongozo huu wa mfukoni (kitabu cha mfukoni) ni chombo cha kazi kinacho lenga kusaidia Polisi kukinga kwa ubora haki za watoto. Inatowa mafasiriyo kuhusu namna gani kutambua kesi za kazi mbaya kwa watoto na namna kuingia kati ili kukinga haki za mtoto. Kwa ajili ya ukingo bora, inahimiza polisi kutumia mazungumzo na ushirika katika kazi zake za kila leo.**

DCAF Le Centre pour la gouvernance du secteur de la sécurité, Genève

THOMSON REUTERS FOUNDATION

OBSERVATOIRE OGP GOUVERNANCE & PAIX

Mwongozo umetolewa kwa lugha ya kifaransa na swahili kwa ushirikiano na DCAF, Thomson Reuters Foundation pia OGP